TANGAZO LA SERIKALI Na. 830 la tarehe 4/10/2024

SHERIA YA KUONDOA MAKABURI,

(SURA YA 72)

# NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 4(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUONDOA MAKABURI, 2024

1. KWA KUWA maeneo yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii yanahitajika kwa ajili ya matumizi ya umma na KWA KUWA kuna makaburi katika maeneo tajwa;

2. Notisi inatolewa kwamba Serikali inakusudia kuyaondoa makaburi hayo na kuyahamishia katika maeneo ya Makaburi ya Halmashauri husika kwa mujibu wa masharti ya Sheria baada ya kuisha kwa siku ishirini na moja (21) tangu kutangazwa kwa Notisi hii;

3. Taarifa kuhusu Makaburi yanayopaswa kuondolewa zimeainishwa katika Jedwali la Pili la Notisi hii na zinaweza kukaguliwa katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi, Dodoma, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa na katika Ofisi za Halmashauri husika;

4. Ndugu wa marehemu waliozikwa katika maeneo hayo anayo haki ya: -

   a) Kuwasilisha kimaandishi kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi pingamizi dhidi ya hatua inayokusudiwa kuchukuliwa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu kutangazwa kwa Notisi hii; na
   b) Kumjulisha Waziri kwa maandishi kuwa, kwa idhini ya Waziri, atahamisha mwenyewe kaburi husika ndani ya miezi miwili tangu kutangazwa kwa Notisi hii.

5. Mapingamizi yote au maombi ya idhini ya Kuondoa Makaburi chini ya aya ya 4 yawasilishwe kwa Waziri kupitia anwani ifuatayo: -

   Katibu Mkuu,
   Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
   Mji wa Serikali- Eneo la Mtumba,
   S.L.P 2908,
   40477 DODOMA

*Tangazo la Serikali Na.830 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 1)*

MAENEO YENYE MAKABURI YANAYOKUSUDIWA KUONDOLEWA

| NA | MKOA | WILAYA | IDADI YA MAKABURI |
|---|---|---|---|
| 1. | LINDI | Ruangwa | 35 |
| Jumla ya Makaburi | | 35 | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

TAARIFA ZA MAKABURI YANAYOKUSUDIWA KUONDOLEWA

| NA | JINA LA MSIMAMIZI | MKOA | WILAYA | KATA | KIJIJI | IDADI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Said Ahmad Liwiku | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 1 |
| 2 | Karim Swalehe Mkangula | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 1 |
| 3 | Safina Husseini Masudi | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 1 |
| 4 | Abdurahaman Swaleh Mkangula | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 2 |
| 5 | Abdallah Said Ngwale | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 3 |
| 6 | Hamadi Omary Chiko | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 4 |
| 7 | Somoe Sefu Mtimwanga | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 5 |
| 8 | Juma Ally Buriani | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 4 |
| 9 | Mohamed Hassan Chikunda | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 5 |
| 10 | Omary Bakari Muhidini | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 5 |
| 11 | Ally Said Chimbanga | Lindi | Ruangwa | Mwembukuru | Nangurugai | 4 |
| | | | | | **Jumla Kuu** | **35** |

Dodoma,
4 Juni, 2024

JERRY WILLIAM SILAA (MB.)
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*